TANGAZO LA SERIKALI NA. 230 la Tarehe 22/3/2019

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)
(SURA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO ZA MWAKA 2019

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usafi wa mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko za mwaka 2019 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo;-

"Ada ya kuondoa taka" Maana yake ni kiwango cha fedha kilichowekwa na Halmshauri kulipia gharama za kuzoa taka kama ilivyofafanuliwa na Sheria Ndogo hizi;

"Afisa Afya" Maana yake ni Afisa yeyote anayesimamia kazi za afya ya mazingira katika Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko;

"Chombo cha taka" Maana yake ni kitu chochote kilichokubalika na Halmashauri ambacho kimewekwa na mwenye jengo husika kwa madhumuni ya kukusanyia taka;

'Duka" Maana yake ni jengo lolote ambapo shughuli ya kununua na kuuza bidhaa mbalimbali zinafanyika hapo;

"Eneo lililo wazi" Maana yake ni eneo linalomilikiwa na Halmashauri ambalo limekatazwa kutumiwa kwa shughuli yoyote ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa;

"Eneo lililozuiwa" Maana yake ni eneo lolote lililo chini ya Halmashauri ambalo Halmashauri limezuilika lisitumike isipokuwa kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko;

"Huduma" Maana yake ni huduma itolewayo na Halmashauri ya

kuzoa taka, kusafisha, kuondoa, kukusanya na kutupa taka za majumbani, biashara na viwandani katika vizimba vilivyojengwa na Halmashauri;

**"**Kaya**"** Maana yake ni familia ya baba, mama, watoto na wategemezi pamoja na mtu yeyote mwenye zaidi ya miaka 18 anayeendesha maisha kwa kujitegemea;

"Kero**"** Maana yake ni kitu chochote ambacho ni chukizo kimewekwa au kujengwa katika hali ya uchafu na kinaweza kuleta adha, harufu mbaya; au Kitu chochote kinachoweza kusababisha magonjwa ya mlipuko na ya kuambukiza, au kinachowez kuleta Madhara kwa maisha ya binadamu na viumbe hai vingine;

**"**Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Kakonko au Afisa aliyeteuliwa nafasi ya Mkurugenzi;

**"**Mmiliki**"** Maana yake ni mtu yeyote anayemiliki eneo au nyumba ya kuishi au ya biashara au nyumba ya kulala wageni;

"Siku ya usafi wa Mazingira**"** Maana yake ni siku maalumu itakayopangwa na Halmashauri ya usafi wa mazingira, itakayohusisha wakazi wote wa Halmashauri kushiriki shughuli za usafi wa mazingira;

**"**Taka Maji**"** Maana yake ni maji yanayotokana na uchafu kutoka vituo vya mafuta, viwandani, majumbani na uchafu mwingine wowote ulio katika hali ya kimiminika au maji machafu yayotiririka ikiwa ni pamoja na kinyesi, mkojo, na matapishi;

"Taka ngumu**"** Maana yake ni taka zote zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara na viwandani pamoja na takataka zote zilizofichama mahali popote zisipostahili, lakini haihusishi maji taka au taka miminika;

**"**Taka za biashara**"** maana yake ni taka zote zitokazo kwenye maeneo ya biashara au viwandani kwa kuzalishwa na viwanda vyenyewe au mahali huduma zinapotolewa ambazo sio kwenye makazi ya watu na hujumuisha taka nyingine zote ambazo sio za majumbani;

**"**Taka za majumbani" maana yake ni taka za kawaida zilizozalishwa kwenye nyumba za kuishi;

**"**Taka za viwandani**"** Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

**"**Taka" maana yake ni takataka zote zinazozalishwa majumbani, kwenye taasisi, sokoni, gengeni, maeneo ya biashara na viwandani pamoja na takataka zote zinazozalishwa mahali popote zisipostahili, mizoga, magari mabovu;

**"**Uchafu hatari" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004;

**"**Wakala" Maana yake ni mzabuni aliyeteuliwa na Halmashauri kutoa huduma zinazohusiana na udhibiti wa taka ngumu au maji taka kwa niaba ya Halmashauri.

4. -(1) Halmashauri itaunda kamati mbalimbali kwa ajili ya kusimamia usafi wa mazingira katika Halmashauri.

(2) Kamati ya usafi wa mazingira ya Halmashauri itajumuisha.

(a) Mganga Mkuu wa Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Afisa Afya wa Halmashauri ambaye atakuwa Katibu;

(c) wajumbe wa kamati ambao ni Muuguzi Mkuu wa Halmashauri, Katibu wa Afya wa Halmashauri, Afisa Mipango miji wa Halmashauri;

(3) Kazi za Kamati ya usafi wa mazingira ya Halmashauri zitakuwa ni;

(a) kuandaa mpango kabambe wa usafi wa Halmashauri;

(b) kupendekeza mbinu mbalimbali zitakazo boresha shughuli za usafi wa mazingira
katika Halmashauri;

(c) kuhamasisha jamii katika kushirika siku ya usafi wa mazingira katika Halmashauri;

(d) kupambana na matumizi mabaya ya mazingira yanayosababisha uchafuzi wa mazingira;

(e) kutoa mapendekezo ya mahali pa biashara, ufugaji na ujenzi ili kuzuia uchafuzi wa mazingira.

(f) kutoa mapendekezo kwa kamati ya usafi na mazingira ngazi ya Kata na Kijiji kuhusiana na masuala ya uhifadhi na usafi wa mazingira.

(g) ) kusimamia kwa jumla masuala ya usafi katika Halmashauri;

(4) Kila mwezi kamati itatakiwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za usafi zinazofanyika kila jumamosi ya kwanza ya mwezi kwa kamati ya watalaam.

Wajibu wa kufanya usafi

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi katika eneo la Halmashauri kufanya usafi wa jumla katika eneo lake lote la makazi au biashara siku moja kwa mwezi kadri itakavyoamriwa na Halmashauri.

(2) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukagua eneo lolote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri kwa nia ya kuangalia kero na kutoa maelekezo ya kuondoa kero hizo.

Marufuku

6. Ni marukufu mtu yeyote kuweka au kutupa taka au uchafu wowote utakaoleta chukizo katika mtaa, uchochoro au eneo lolote lililokatazwa na Halmashauri.

Chombo cha kukusanyia taka

7.-(1) Mtu yeyote anayemiliki nyumba au mpangaji wa nyumba anatakiwa kuwa na chombo cha kukusanyia taka chenye ukubwa unaotosheleza na kiwe na mfuniko unaofaa au awe na shimo la takataka.

(2) Ukusanyaji wa taka ngumu utafanywa na Halmashauri au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Halmashauri na ada ya uzoaji taka itatozwa kwa mujibu wa viwango vilivyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(3) Itakuwa ni wajibu wa mmiliki mpangaji wa nyumba kufagia na kuondoa uchafu au malundo na kuweka safi eneo lote la nyumba yake.

(4) Vichochoro vyote vitatunzwa na wenye nyumba husika na kila mwenye nyumba au mpangaji atawajibika kutunza eneo linaloangukia kwake yaani kila nyumba itakuwa na kijisehemu katika uchochoro huo.

Vyombo vya taka kwenye mabasi

8.-(1) Kila mwenye basi la abiria litakaloingia eneo la Halmashauri atawajibika kuwa na chombo cha kuhifadhi taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka katika chombo hicho.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote nje ya basi lake, barabarani au stendi.

Kutiririsha maji

9. Ni marufuku mtu yeyote kumwaga, kutiririsha maji taka katika mtaa, uchochoro, eneo la wazi, mtaro uliowazi au mashimo yasiyoruhusiwa.

Shimo la maji taka

10.-(1) Utakuwa ni wajibu wa kila mwenye nyumba kuwa na shimo la kuhifadhia maji taka.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuoga au kufulia kwenye chanzo cha maji, mto au mfereji au tangi ambalo halikuwekwa kwa madhumuni hayo.

(3) Endapo kutatokea kero zinazosababishwa na maji taka katika nyumba yenye mpangaji au wapangaji na iwapo mwenye nyumba hawezi kupatikana kwa haraka, Halmashauri inaweza kufanya usafi katika eneo hilo ili kuondoa taka hizo na gharama hizo zitafidiwa na mwenye nyumba pindi akipatikana.

Vyoo

11.-(1) Mtu yeyote anayemiliki nyumba ya makazi anatakiwa aweke vyoo vya kutosha kwa idadi ya watu watakaoishi humo.

(2) Mtu yeyote anayemiliki kiwanda, mgahawa, shule za bweni, shule ya kutwa, hoteli au jengo lolote la umma, sehemu za burudani, au nyumba yoyote anatakiwa kuweka vyoo vinavyoridhisha kwa ajili ya matumizi ya wanaume na wanawake na atahakikisha vyoo hivyo vina mwanga na hewa ya kutosha.

(3) Kila mgahawa wa vyakula au vinywaji ni lazima uwe na vyoo vya kutosha kwa ajili ya wateja na watumishi wa Mgahawa huo.

Uanzishwaji wa Hosteli

12.-(1) Ni marufuku mtu yeyote kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni au hosteli ya wanafunzi bila ya kibali cha Halmshauri.

(2) Kibali cha hosteli ya wanafunzi au nyumba ya wageni kitatolewa kwa kuzingatia yafuatayo:-

a) mwanga na hewa ya kutosha;
b) nafasi ;
c) vifaa (samani) vya kutosha;
d) uimara wa jengo;
e) uhifadhi na uondoshaji wa maji taka na taka ngumu;
f) usafi wa jumla wa majengo na vifaa vyake; na
g) Utoshelezaji wa vyoo na bafu kwa jinsia zote.

Marufuku kutumia vyoo vibovu

13. Choo cha aina yoyote ambacho kwa maoni ya Halmashauri kitaoonekana kichafu au kuhatarisha maisha ya binadamu, hakitaruhusiwa kutumika mpaka hapo Halmashauri itakaporidhika na matengenezo yaliyofanyika.

Uchimbaji mashimo ya maji taka

14.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote bila kupata idhini ya Halmashauri ya maandishi na katika mchoro wa jengo hilo lazima lionyeshe sehemu ya kuchimba shimo la kuhifadhi maji taka kutoka kwenye nyumba au jengo hilo.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kusababisha au kuruhusu eneo la nyumba anayoishi kuwepo uchafu wa takataka au majani marefu.

(3) Itakuwa ni wajibu wa mmiliki au mpangaji wa nyumba kufagia na kuondoa uchafu au malundo ya taka na kuweka safi eneo lote la nyumba yake.

Utupaji wa maji taka za Viwanda

15.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha kiwanda chochote kinachotoa maji taka bila ya kuwa na mitambo ya kusafishia maji taka hayo ambayo imeidhinishwa na Halmashauri.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuruhusu maji taka kutoka viwandani, au eneo lolote linalofanya utengenezaji kuingia katika vyanzo vya maji, ardhini, maeneo ya wazi, uchochoro, mitaro iliyo wazi.

Ni marufuku kutelekeza magari mabovu

16.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutelekeza magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa au vichochoro au mitaro iliyo wazi na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kutengeneza gari au mtambo eneo ambalo siyo mahususi kwa shughuli hiyo au eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri.

Halmashauri au Wakala kukusanya na kutupa taka Ngumu

17.-(1) Halmashauri inaweza kuweka Wakala atakayefanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa maeneo ya katikati ya Vitongoji, Vijiji na Kata.

(2) Wakala atawajibika kukusanya taka ngumu na kuzipeleka kwenye jalala na kukusanya Ushuru wa taka ngumu kwa wazalishaji wa taka katika maeneo anayotoa huduma.

(3) Wakala ataingia Mkataba na Halmashauri wa kukusanya taka ngumu katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya na kudhibiti taka ngumu kama itakavyoelekezwa na Halmashauri katika Mkataba huo.

Taka za Nyumbani

18.-(1) Kila mkazi au mpangaji kwenye nyumba ya makazi atawajibika kuweka chombo cha kuridhisha cha kuweka taka za majumbani chenye uzajo unaoridhisha na chenye mfuniko unaofaa na kuhakikisha kuwa takakata zote zinazozalishwa kwenye nyumba hiyo zinawekwa humo kila siku.

(2) Takataka hizo zitatolewa nje pindi gari la kusomba taka linapopita au kupelekwa kwenye ghuba za taka zitakazowekwa mitaani.

Taka za biashara

19. Kila mkazi kwenye nyumba ya biashara au mpangaji atalazimika kuweka chombo cha kuhifadhi taka za biashara chenye ujazo wa kuridhisha cha kuhifadhi taka za biashara chenye mfuniko wa kubana na kuhakikisha kuwa taka zote zinahifadhiwa kwenye chombo hicho chenye ujazo wa kutosheleza.

Ujenzi au karabati Nyumba

20.-(1) Hairuhusiwi mtu au kikundi cha watu kubomoa jengo lolote kwa nia yoyote ile bila kupata kibali cha Halmashauri.

(2) Kila anayetaka kubomoa nyumba atatakiwa kuomba kibali cha kubomoa nyumba kutoka Halmashauri.

(3) Kibali cha kubomoa kitatolewa kwa ajili ya gharama za kuondoa vifusi na mabaki ya kubomoa kwa kadri itakayokuwa imetathminiwa na Halmashauri.

(4) Mtu yeyote anayetaka kujenga au kukarabati jengo lolote atatakiwa kuhifadhi vifusi na vifaa vingine vya ujenzi ndani ya eneo au kiwanja chake.

Utaratibu wa kukusanya taka

21.-(1) Halmashauri itaweka mipango na utaratibu wa ukusanyaji na utupaji taka kutoka kwenye sehemu za biashara na nyumba za kuishi na kuzizoa taka hizo na kuzitupa.

(2) Halmashauri inaweza kufanya kazi ya kukusanya na kutupa taka yenyewe au kuteua Wakala kwa makubaliano maalum.

(3) Kiwango cha juu cha taka zitakazokusanywa kutoka katika eneo la makazi au taasisi au Kampuni moja hakitazidi tani nne.

(4) Kiasi chochote kitakachozidi tani nne, mhusika atatakiwa kulipia gharama nyingine kwa Halmashauri au Wakala.

(5) Kiwango cha fedha itakayolipwa na mhusika wa kuzalisha taka zaidi ya tani nne kwa mujibu wa kifungu kidogo cha kifungu hiki kitapangwa na Halmashauri au Wakala kutegemea umbali kutoka eneo ulipo uchafu hadi sehemu ya kutupa.

(6) Kukusanya taka kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa na maana ya kuzoa taka zilizokusanywa pamoja na mzalishaji wa taka hizo katika eneo la barabara ya jirani na eneo lake ambayo gari la taka hupita.

Ufungaji wa mazao au vitu vinavyoweza kuoza kwa haraka

22. Mzalishaji yeyote, mfanyabiashara au mchuuzi wa mazao au vitu vinavyoharibika au mtu yeyote anayejishughulisha na mazao au vitu vinavyobaribika au kuoza kwa haraka haruhusiwi kuingiza sokoni vitu hivyo vikiwa vimefungwa au kufunikwa kwa majani, matawi ya miti au aina nyingine yoyote ya sehemu ya mmea.

Ufugaji mitaani

23.-(1) Kila mfugaji wa ng’ombe, mbuzi, kuku, nguruwe na wanyama wengine wa nyumbani atawajibika kukusanya na kuhifadhi uchafu utokanao na wanyama hao kabla na baada ya kuchinjwa.

(2) Uchafu utokanao na ufugaji huo kama vile nyasi au mabaki ya vyakula vyao vitadhibitiwa na mfugaji katika hali ambayo itairidhisha Halmashauri na ambayo haitaleta kero kwa jamii.

(3) Kila atakayetaka kufuga wanyama waliotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki ni sharti awe na eneo la

kutosha la na apate kibali cha Halmashauri.

(4) Ni marufuu kwa mfugaji kuruhusu mifugo kuzurura hovyo barabarani au katika eneo lolote la Mji.

Uteuzi wa Wakala wa kukusanya na kutupa taka

24. Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kukusanya ushuru wa taka kuzoa taka na inaweza kuingia naye Mkataba wa kufanya kazi za ukusanyaji na uzoaji taka.

Wajibu wa mmiliki wa eneo kuondoa taka

25.-(1) Iwapo kero itaonekana mahali pa karibu na makazi kwa sababu ya biashara au taka za majumbani kutupwa eneo la makazi Halmashauri itampa ilani mmiliki au mkazi anayeishi kwenye nyumba hiyo na kumtaka aondoe kero hiyo kwa muda utakaotajwa katika ilani na iwapo muda aliopewa katika ilani utamalizika, kero ikawa inaendelea atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote mmiliki wa kiwanja chochote au sehemu ya kiwanja ambacho hakikuendelezwa au kwa mtu mwenye kiwanja ambacho hakina wakazi au kuendelezwa kutupa takataka ya aina yoyote katika eneo hilo.

Wajibu wa kupima Afya

26. Kila mtoa huduma katika nyumba ya kulala wageni, hoteli, mgahawa,wauzaji wa duka la kuuza nyama, baa na vilabu vya pombe atatakiwa kupima afya kila baada ya miezi mitatu na kila muhudumu atalipa kiasi cha shilingi elfu tano tu.

Jukumu la Halmashauri

27.-(1) Halmashauri itawajibika kuhamasisha uundaji wa vyama vya kiraia (CBO's), kuvitambua vyama hivyo, kuvipa nguvu za kufanya kazi kisheria na kuviwezesha kuanza kufanya kazi.

Jukumu la Wakala wa kukusanya na kutupa taka

28.-(1) Halmashauri inaweza kuweka wakala atakayefanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa maeneo ya miji midogo au katika mitaa au Kata.

(2) Wakala atawajibika kukusanya taka ngumu na kuzipeleka kwenye jalala na kukusanya Ushuru wa taka ngumu kwa wazalishaji wa taka katika maeneo anayotoa huduma.

(3) Wakala ataingia mkataba na Halmashauri wa kukusanya taka ngumu katika mji na kudhibiti taka ngumu kama atakavyoelekezwa na Halmashauri katika mkataba huo.

Makosa

29. Itakuwa ni kosa kwa Mtu yeyote,kampuni,mfanyabiashara, taasisi, ambaye:-

a) atamzuia Afisa Mwidhiniwa kukagua nyumba mgahawa, karakana viwanda, nyumba ya biashara, au taasisi;
b) atashindwa kuzingatia kanuni za afya;
c) atatupa au kuchoma taka hovyo;
d) ataweka magari mabovu kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;
e) atatupa taka kwenye kiwanja ambacho hakijaendelezwa, barabarani au eneo lililo la wazi;
f) ataelekeza maji machafu kenye chanzo cha maji;
g) atafunga mitambo au vyombo vya usafiri vinavyochafua hewa kwa kutoa moshi mzito; au

Adhabu

30. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

31. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza kiasi cha fedha mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi kisichozidi shilingi laki moja (100,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari yake mwenyewe na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetungwa chini ya Kifungu cha 7 (2)*)

ADA ZA HUDUMA ZA USAFI NA UZOAJI WA TAKA

| NA | ENEO | ADA ZA UZOAJI TAKA |
|---|---|---|
| 1 | Viwanda vikubwa/ Taasisi | 240,000/= kwa mwaka |
| 2 | Viwanda vidogo | 120,000/= kwa mwaka |
| 3 | Hoteli | 60,000/= kwa mwaka |
| 4 | Mgahawa | 36,000/= kwa mwaka |
| 5 | Duka la jumla | 36,000/= kwa mwaka |
| 6 | Biashara nyinginezo | 24,000/= kwa mwaka |
| 7 | Nyumba za kuishi | 12,000/= kwa mwaka |
| 8 | Kutupa uchafu katika eneo ya dampo | 5,000 /=kwa tripu |

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha (31))*

(HATI YA KUKIRI KOSA**)**

Mimi…………………………………………………………….wa S.L.P ………….nakiri kupatikana na kosa la………………………..kinyume na Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko za mwaka 2018. Nimekubali kulipa Tshs……………........................................................................kama adhabu ya kosa hilo na nimepewa stakabadhi Na………………ya tarehe…………………………

Sahihi ya Mkosaji…………………………………
Jina la mkosaji…………………………………….

Sahihi ya Afisa wa Halmashauri……………………………………
Jina la Afisa wa Halmashauri……………………………………….
Tarehe …………………………………………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ilibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 24/01/2015 na nembo hiyo imebandikwa mbele ya:-

……………………………………………..
MASUMBUKO S. MAGAG'HILA
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko

**L.S**

…………………………………………………
MHE. JUMA MAGANGA
Mwenyekiti wa Halmashauri
Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko

NAKUBALI,

Dodoma,
01 Machi, 2019

… ……………………………………….
SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*